

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



## WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

### MWONGOZO WA UPIMAJI WA COVID-19 KWA WATU WANAOSAFIRI NJE YA NCHI.

Toleo la Kwanza, 20 Julai 2020

#### 1.0 Utangulizi:

Mlipuko wa ugonjwa wa COVID-19 umeendelea kuziathiri nchi mbalimbali toka ulipothibitika mwezi desemba, 2019. Hadi kufikia tarehe 23 June 2020 jumla ya wagonjwa 8 993 659 na vifo 469 587 vimeripotiwa. Nchi mbalimbali zimeweka mikakati mbalimbali ikiwemo katazo la kutoka nje pamoja na kuzuia safari za Kimataifa. Tanzania ni miongoni mwa nchi ambazo zimeripoti ugonjwa huu na kuchukua hatua madhubuti kudhibiti maambukizi, hali ambayo imepelekea kupungua kwa wagonjwa wa COVID-19.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imefungua anga lake ili kurejesha usafiri wa kawaida unaojumisha ndege za biashara na abiria kwenda kwenye nchi mbalimbali. Kutokana na hali hiyo, Wizara imeandaa mwongozo wa kuwapima wasafiri wanaokwenda nje ya nchi hususan zile zenye hitaji la kupimwa maambukizi ya COVID-19. Mwongozo huu unalenga kuweka utaratibu wa upimaji wa wasafiri kwa hiari kwa wanaohitaji kwenda kwenye nchi ambazo zinahitaji wawe wamepima kabla ya safari zao.

#### 1.1 Maeneo ya Mwongozo:

Mwongozo huu unaweka utaratibu wa maombi, upimaji, namna ya kupata majibu, uhakiki mipakani na gharama za upimaji.

#### 1.2 Utaratibu wa Maombi na Upimaji:

- 1.2.1 Msafiri aelimishwe kupata taarifa kutoka katika ofisi za ubalozi wa nchi anayotaka kwenda juu ya uhitaji wa kupimwa ugonjwa wa COVID-19.
- 1.2.2 Msafiri atakayehitaji huduma ya upimaji ugonjwa wa COVID-19 afike katika Hospitali ya Mkoa akiwa na uthibitisho wa uhitaji wa kupima kwa nchi anayotaka kwenda ikiwemo hati ya kusafiria.

- 1.2.3 Ofisi ya Mganga Mkuu wa Mkoa isimamie zoezi hili ikiwemo uchukuaji wa sampuli za msafiri na kuzituma katika Maabara Kuu ya Taifa.
- 1.2.4 Sampuli za wasafiri zainishwe vizuri kwa kuandika maneno ya jina la Mkoa\_ITR (International Traveller).
- 1.2.5 Msafiri aelimishwe kupima siku tano kabla ya siku ya kusafiri kwa sababu cheti cha COVID-19 kitadumu kwa muda wa siku 14 au itategemea masharti ya nchi husika wanapokwenda.

### **1.3 Utaratibu wa kupata majibu na kupewa vyeti:**

Majibu ya vipimo yatatumwa kwa Mganga Mkuu wa Mkoa ambaye kwa wale ambao watakuwa hawana maambukizi watapewa vyeti. Majibu yatatolewa ndani ya saa 72. Wasafiri wote waliopewa vyeti majina yao yatatumwa mipakani kwa ajili ya uhakiki.

### **1.4 Uchunguzi/ uhakiki wa vyeti mipakani:**

Wasafiri ambao wanavyeti vya COVID-19 washauriwe kuwa vyeti vyao vitakamilika baada ya kugongewa mihuri na kuhakikiwa mpakani (verification). Utaratibu huu unaweza kufanyika kwa njia ya kielektroniki.

### **1.5 Gharama za upimaji:**

Gharama za vipimo vya COVID-19 zitakuwa kama ifuatavyo kwa kila safari;

- Raia wa Tanzania: Tsh.40,000/=
- Raia Mkaazi wa Tanzania: Tsh.60,000/=
- Raia wa Kigeni: USD.100

**N.B: Malipo haya yalipwe katika akaunti ya Serikali ya Huduma za Afya Mipakani na wahusika wapewe stakadhi za Serikali za kielektroniki.**

Mwongozo huu utaboreshwa kulingana na mahitaji.



Umyy Mwalimu (MB)

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA WAZEE NA WATOTO**